Ijumaa 15 Januari 2021
www.timesmajira.co.tz

Huduma za meli Ziwa Nyasa zitakavyochochea ukuaji uchumi Ruvuma

Na Albano Midelo

■ ■ WAZIRI mkuu Kassim Majaliwa aliziindua meli mpya ya abria inayoitwa MV Mbeya II kwenye Ziwa Nyasa, ambayo itakuwa inahudumia bandari zilizoko katika wilaya za Kyela mkoani Mbeya, Ludewa mkoani Njombe na Nyasa mkoani Ruvuma.

Akitoa taarifa ya huduma za bandari kwenye Ziwa Nyasa, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Mhandisi Deusdedit Kakoko, alisema kuwa TPA wanahudumia idadi ya bandari 15 kwenye ziwa Nyasa, ambapo katika Mkoa wa Ruvuma wanahudumia bandari sita.

Alitaja bandari za Ziwa Nyasa mkoani Ruvuma kuwa ni Mbambabay, Luli, Njambe, Lundu, Mkili na Ndumbi.

Pia, alendelea kutaja bandari za ziwa hilo mkoani Njombe, ambazo TPA pia wanahudumia kwamba ni sita, ambazo ni Lumbila, Itungi, Nsisi, Makonde, Lupingu na Manda.

Mkoa wa Mbeya, alitaja bandari tatu ambazo ni Itungi, Kiwira na Matema, ambazo pia TPA wanahudumia.

Mhandisi Kakoko alisema kuwa, katika baadhi ya bandari TPA wameweka miundombinu ya kisasa, kwamba pia kuna bandari ambazo zinaendelea kuwekwa miundombinu kwa ajili ya utoaji huduma bora na za kisasa kwenye bandari hizo.

"Kila bandari inahitaji kuwa na magati, maghala, yadi za kutunza mitambo na mizigo na uwepo wa nyumba za kuishi wafanyakazi, sanjari na kuweka mfumo ya zimamoto, mashafi, maptaka na mfumo ya TEHAMA ili kufanyakazi kwa ufanisi na tija kulingana na maelekezo ya serikali," Mhandisi Kakoko alisisitiza.

Alisisitiza kuwa, katika maka mitano iliyo TPA wameppanga kukamilisha miundombinu na mfumo yote kwenye bandari zote 15 zilizopo kwenye Ziwa Nyasa.

Akizungumzia utendajikazi wa TPA kwenye Ziwa Nyasa kwa kipindi cha maka mitano iliyopita, Mhandisi Kakoko alitaja shehena kuu zilizokuwa zinasafirishwa kuwa ni mkaa ya mawe ambayo ilikuwa inapakiwa kutoka bandari za Ndumbi na Mbambabay na kusafirishwa hadi Bandari ya Kiwira Kyela mkoani Mbeya.

Alisema kuwa, katika kipindi hicho, TPA pia alweza kusafirisha saruji, mabati, darjaa, sukari na mizigo mingine, ambapo kwa kipindi cha maka sita iliyopita ilisafirishwa shehena ya mizigo zaidi ya tani 4,500 kwa mwaka.

Mhandisi Kakoko alisema kuwa, kwa ujumla kulikuwa na ongezeko la tani 9,000 kutoka tani 2,233 ya mwaka 2014/2015 hadi tani zaidi ya 11,000 mwaka 2019/2020.

Mhandisi Kakoko anasisitiza kuwa ili kuboresha huduma katika bandari zote za ziwa Nyasa, TPA inatekeleza mpango kabambe unaoanza mwaka 2021/2022 na unaolenga kukamilika katika kipindi cha mwaka 2028/2029.

"Mpango huo kabambe utaongeza shehena ya mizigo katika Ziwa Nyasa kutoka tani zaidi ya 11,000 hadi kufikia shehena ya mizigo zaidi ya tani 100,000, lengo hili linachochewa na mpango mizuri ya serikali, ikiwemo kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya lami toka Mbinga hadi Mbambabay," alisema.

Alisema kuwa, kutokana na kukamilika kwa lami kwenye barabara ya Mbinga hadi Mbambabay na kuanza kutoa huduma za meli kwenye Ziwa Nyasa, itafufua uchumi wa mji wa Mbambabay, hivyo kuunganisha Tanzania kupitia ushoroba wa Mtwara na nchi za Malawi, Msumbiji na Zimbabwe na Zambia.

"Mji wa Mbambabay utafufuka kwa kasi, TPA inafanya usanifu wa bandari zote zilizopo katika ziwa Nyasa na kwa kweli tunashirikiana na nchi jirani ya Malawi ili wakati tunaendeleza bandari za Tanzania, tuendeleze pia bandari za Malawi.

"Pia tunafanya kampeni za masoko katika nchi za Malawi na Msumbiji," Mhandisi Kakoko alisema.

Akizungumzia kuhusu meli mpya kwenye Ziwa Nyasa, mkurugenzi huyo alisema kuwa Ziwa Nyasa sasa lina meli tatu zinazomilikiwa na serikali, kwamba kati ya hizo meli mbili za MV Njombe na MV Ruvuma ni za mizigo, na meli moja ya MV Mbeya II ni ya abria.

Alisema kuwa, katika kipindi cha maka sita iliyopita kwa wastani kwa mwaka kulikuwa tie abria 4,917 amesema kumbe kuwa na ongezeko la abria katika mwaka 2019/2020 kwa abria 894 mwaka 2018/2019 ndi abria 3,867 mwaka 2019/2020 baada ya kujitokeza meli ya abria ya MV Chambro ya Msumbiji ambayo ilanza kutoa huduma baada ya kuzuka Ugonjwa wa COVID-19 maarufu Corona.

Hataheyo alisema kuwa idadi ya abria inatarajia kuongezeka kwenye Ziwa Nyasa baada ya kuzindulwa kwa huduma ya meli ya abria ya MV Mbeya II ambayo itawezesha kusafirisha abria zaidi ya 12,000 kila mwezi.

Akizungumzia gharama za meli zote tatu kwenye Ziwa Nyasa, Mkurugenzi Mkuu TPA huyo alisema kuwa zaidi ya shilingi bilioni 20.1 zimetolewa na serikali kujenga meli zote tatu, na kwamba meli hizo zimetengenezwa na Kampuni ya Songoro Marine inayomilikiwa na Mtanzania.

"Meli mbili za mizigo MV Njombe na MV Ruvuma kila moja ina uwezo wa kubeba tani 1,000 na kwamba kila meli imegharimu shilingi bilioni 5.5.

"Na meli ya abria ya MV Mbeya II ina uwezo wa kubeba abria 300 na mizigo tani 200, imegharimu shilingi bilioni 9.1," alisema.

Mhandisi Kakoko alisema kuwa, meli ya abria ya MV Mbeya II imethi pia la meli ya MV Mbeya I iliyozama eneo la Makonde ziwani Nyasa mwaka 1977.

Hata hivyo, alisema kuwa Meli ya MV Mbeya II baada ya kujengwa dingdwa majini Septemba 2019, na kwamba kwa kuwa meli ni chombo ambacho kinatakwa kuwa na usalama wa kutosha kikaguliwa kimataifa na kupata kibali cha mamlaka inayosimamia usalama wa vyombo vya majini na kutoza safari Oktoba 20, 2020.

Akizungumza baada ya kuzindua meli mpya ya abria ya MV Mbeya II waziri mkuu Kassim Majaliwa alisema kuwa Wilaya ya Nyasa sasa imefunguka kutokana na kukamilika kwa usalama wa barabara ya lami toka Mbinga hadi Mbambabay, na kuanza rasmi kwa huduma za meli tatu ndani ya Ziwa Nyasa.

Waziri mkuu alisema kuwa, serikali imetoa fedha za ujenzi wa meli tatu katika Ziwa Nyasa, na kwamba kati ya kujenga meli ni endeleu na inafanyika katika maziwa yote kwa kuwa bandari ni lango kuu la kuleta uchumi wa taifa.

Majaliwa alitaja sizna ya serikali ya awamu ya tano kwamba, ni kuhakikisha Watanzania wanafanya biashara katika mazingira rahisi, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji ili kuchochea shughuli za uchumi na uzalishaji.

"Ujenzi wa meli ya abria na umaishaji wa bandari katika Ziwa Nyasa una lengo la kumarisha shughuli za kuchumi [illegible] biashara na uwekezaji [illegible] bandari wa Ziwa Nyasa.

[illegible] serikali tumepania [illegible] watanzania [illegible] bandari kuwanufaikiwa [illegible] ujenzi wetu," [illegible] alisisitiza.

[illegible] mkuu alitoa rai kwa [illegible] wakopo ndani na nje [illegible] kuwekeza Wilaya [illegible] ambako miundombinu yake imeboreshwa, ikiwemo barabara ya lami, umeme na usafiri wa majini.

Mkuu wa Mkoa (RC) Ruvuma, Christina Mndeme, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Nyasa, alipongeza serikali kwa kutoa mahiore ya fedha kujenga meli tatu mpya kwenye Ziwa Nyasa.

RC Christina alisema kuwa, kukamilika na kuanza safari kwa meli ya abria ya MV Mbeya II na kukamilika kwa barabara ya lami ya Mbinga hadi Mbambabay itaondoa kabisa kero ya usafiri na usafirishaji ilyokuwa inawapata wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

"Sasa Mtanzania anaweza kusafiri kutoka Dar es Salaam hadi Mbambabay kwa kutumia barabara au meli bila kugusa vumbi huyu ndiye Dkt. John Magufuli, sasa Mkoa wa Ruvuma unakwenda kuonekana majini,nchi kavu na angani," RC Christina alisisitiza.

RC Christina alisisitiza kuwa, uwepo wa miundombinu hiyo itachochea shughuli za biashara na utali, kwa sababu Mkoa wa Ruvuma umebarikiwa kuwa na vivutio adimu vya kitali, ikiwemo fukwe na visiwa kwenye Ziwa Nyasa.

Mhandisi Stella Manyar ra, M'bunge Jimbo la Ny sa, amesema kuwa, kuboresi ra kwa barabara na uwepo wa r eli mpya vitaongeza idadi ya wageni wanaotembelea wilaya Nyasa ambako ni kitovu cha utali katika Mkoa wa Ruvuma.



Abiria wakitoka kwenye Meli ya Mv Mbeya II baada ya kutia nanga Bandari ya Mbambabay wilayani Nyasa. (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner